# Bilioni 20/- zajenga machinjio

Na John Mhala, Longido

WAFANYABIASHARA wa mifugo wilayani Longido katika Mkoa wa Arusha, wataachana na adha ya kwenda Kenya kuchinja mifugo yao, baada ya serikali kujenga machinjio kwa Sh bilioni 20 wilayani hapa.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Dk Jumaa Mhina, alisema hayo katika mahojiano maalumu na HabariLEO wilayani hapa.

Alisema wafanyabiashara wa mifugo walikuwa wakipata adha kwani kila siku walikuwa wakipeleka mbuzi zaidi ya 3,000 katika machinjio nchini Kenya.

Kwa mujibu wa Dk Mhina, adha hiyo sasa itakuwa historia baada ya serikali kuwajali na kujenga kiwanda hicho kikubwa na cha kisasa katika Wilaya ya Longido ili kukidhi mahitaji ya wafugaji.

Alisema kiwanda hicho kimeshakamilika na wakati wowote kitaanza kazi na kwamba, kitaongeza mapato ya halmashauri na kuvuka malengo ya makusanyo waliyokusudia.

Dk Mhina alisema Wilaya ya Longido ina fursa nyingi za kibiashara na kwamba, wafanyabiashara pia wanaweza kufungua viwanda vingi kama kiwanda cha ngozi, maziwa na nyama ili wafugaji wanufaike zaidi na mifugo yao.

Alisema Longido kuna maeneo makubwa hivyo wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi waende kuwekeza kwani watapewa kipaumbele.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alisema kujengwa kwa kiwanda hicho kunatoa fursa kubwa kwa wafugaji na wafanyabiashara wilayani Longido kwani kutawawezesha kufanya biashara yao kwa uhakika zaidi na kujiingizia kipato.

Aliwataka wafugaji wilayani wanaokisiwa kuwa takriban asilimia 99, kutopeleka mifugo yao Kenya na badala yake, wapeleke katika kiwanda hicho ili serikali ipate mapato yake.

Alisema Rais John Magufuli hakufanya makosa kutoa pesa na kujenga kiwanda hicho katika Mji wa Longido kwani aliona adha ya wafanyabiashara wa mifugo wanayopata wanapohitaji huduma hiyo, hivyo wamuunge mkono.

Scanned with CamScanner

# Dar fish sellers feel pinch of the Covid-19 pandemic

By Blandina Semwaiko, TUDARCo

TRADERS selling fried fish at the Ferry Market in Dar es Salaam have decried lack of customers due to impact of Covid-19 pandemic.

They said before the pandemic, they used to sell fish to foreigners, but now there are nowhere to be seen.

"We're currently facing hard times as there are no more big customers who used to buy fish because of the virus. The outbreak of Coronavirus spoiled our business as sometimes, Chinese were among the best customers of fish at this market, but now they aren't coming as it was in the past," said Amisi Juma, a fish trader at the fish market.

"To be honest, things are not pleasing these days; the business is so difficult here as there are no many customers as it was used to be. The outbreak of Coronavirus has spoiled our business. There are no longer foreigner customers who used to come here, Chinese were among the best customers at this market," said Hamis Juma, one of the fried fish traders.

Hamis said that presently, traders can stay from morning till evening without selling anything, something which affects them deeply as they have families to take care of as well as to pay rent for the business area.

He added that before corona, customers from Uganda and Turkey were able to meet retailers and buy large quantities of fish for export to their countries, but now it is different from how it was before.

For her part, Zaran Omary, also a fish trader at the market hinted that during corona crisis, sales have dropped and traders are earning little.

The traders further asked the government to establish more fish processing factories in Dar es Salaam so as to benefit not only the fish sellers but the nation as well.

"The government should establish fish processing factories in the country for the development of Tanzanian fishermen, for example in Dar es Salaam, there is very few fish processing factories," Zarau added.

> **To be honest, things are not pleasing these days; the business is so difficult here as there are no many customers as it was used to be. The outbreak of Coronavirus has spoiled our business**